**MAJUMUISHO YA MAPENDEKEZO YA TAASISI ZA DINI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA MCHAKATO WA MABADILIKO YA KATIBA, 2011**

**Utangulizi**

Wawakilishi wa taasisi za dini mbalimbali nchini, waliokutana chini ya mwavuli wa Baraza la Mashirikiano ya Dini Mbalimbali kwa ajili ya Amani Tanzania (IRCPT), mjini Dar es Salaam (Novemba 1-2, 2011), kwa lengo la kupitia mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011, wamepitisha mapendekezo kama inavyoelezwa katika waraka huu.

Kwa ujumla kumekuwepo na maboresho katika Mswada wa sasa wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ukilinganisha na Mswada uliotolewa awali. Hata hivyo bado kuna dosari kadhaa ambazo zinahitaji maboresho zaidi kama ifuatavyo:

**1. Jina la Mswada**

Kuna kukinzana kwa tafsiri ya tamko la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuandikwa kwa katiba mpya ya Tanzania na jina la Mswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Inapendekezwa kuzingatia tamko la Rais la kuandikwa kwa Katiba mpya.

**2. Tafsiri ya Neno ‘Serikali’**

Katika utangulizi neno Serikali halijapatiwa tafsiri na kuleta utata kati ya ‘*Governmen*t’ na ‘*Executive’.* Inapendekezwa kuandikwe tafsiri ya neno Serikali ili kuepusha upotoshaji au tafsiri zinazotofautiana.

**3. Madhumuni ya Mswada**

Kwenye Madhumuni ya Sheria kinakosekana kipengele kinachotamka wazi wazi kuwa moja ya Madhumuni ya Mswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ni kuanzishwa kwa mchakato wa kuandika Katiba mpya. Inapendekezwa kipengele hicho kiongezwe.

**4. Uteuzi wa Wawakilishi wa Makundi**

Inapendekezwa kuwa jukumu la kuteua wawakilishi wa Makundi liachwe kwa makundi yenyewe.

## 5. Hadidu Rejea

Inapendekezwa kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano lishiriki kuandaa hadidu rejea. Hadidu rejea hizo ziwekwe wazi kwa wananchi.

## 6. Uratibu wa Mchakato

Uratibu wa mchakato wa Katiba haujawekwa wazi hasa ushiriki wa pande mbili za Muungano. Hatari yake ni kwamba, endapo upande mmoja wa Muungano hawatapiga kura kwa asilimia 50 kwenye kura ya maoni au theluthi mbili kwenye Bunge la Katiba, mchakato wa Katiba mpya utakwama.

Inapendekezwa;

a). Wapiga kura wote katika kura za maoni wapige bila kujali wametoka upande gani wa muungano, bara au Zanzibar, ili asilimia 50 ilete maana halisi;

b). Wajumbe wote wa Bunge la Katiba wapige kura bila kujali wametokea upande upi wa Muungano, bara au Zanzibar, ili theluthi mbili ilete maana halisi.

c). Endapo katika (a) au (b) hapo juu kura hazitafikia kiwango kilichowekwa, Hadidu rejea mpya ziandaliwe.

## 7. Muda wa kukamilika kwa mchakato

Mswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba haujabainisha muda wa mtiririko mzima wa zoezi hili. Inapendekezwa ukomo wa muda uwekwe kwenye mtiririko wa mchakato wa kukusanya maoni ili kuepuka kuwa na mchakato kwa muda usiojulikana na kuleta uwajibikaji. Sambamba na hilo, kuna haja ya kuelekeza nguvu kazi pamoja na rasimali za kutosha kwenye hatua zote za mchakato ili Katiba inayoridhisha wananchi ipatikane .

## 8. Haki za Binadamu

Haki isiyotekelezeka ni haki bandia na ni muhimu haki zote zilizoainishwa katika Katiba kuwekwa ndani ya Katiba na kuziwekea utaratibu wa kuzitekeleza. Inapendekezwa suala hili pia lishughulikiwe katika mchakato wa kuunda Katiba mpya.

## 9. Jinsia

Suala la uwakilishi wa kijinsia halikuzingatiwa katika mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Inapendekezwa suala hilo lifanyiwe kazi ili kuwepo uwiano wa kijinsia ulio sawa.

## 10. Makosa ya Jinai kwenye mchakato

Mswada wa Sheria umeibua makosa pamoja na adhabu atakayopewa mtu anayekwamisha majukumu ya Tume au wajumbe wake kufanya kazi. Hatari ya hatua za aina hii ni kuleta hofu miongoni mwa wananchi wa kawaida na inaweza kupelekea kususa ushiriki. Inapendekezwa kipengele hiki kifutwe, kwani tayari zipo adhabu zilizoainishwa kwenye Sheria ya Makosa ya Jinai (yaani *Penal Code*) kushughulikia mambo kama hayo.

## 11. Mamlaka ya Rais

Kwa kuzingatia madaraka makubwa aliyopewa Rais na Katiba ya sasa, inapendekezwa kuangalia na kuweka mfumo mbadala unaojitegemea katika kusimamia mchakato wa kukusanya, kuainisha na kupitisha maoni juu ya mchakato wa kuandaa Katiba mpya.

## 12. Misingi Mikuu ya Kitaifa na Maadili ya Jamii

Kuna mambo kadhaa ambayo tume inatakiwa kuyazingatia. Inapendekezwa kwamba wananchi wapewe fursa ya kutosha kuyajadili. Miongoni mwa hayo ni pamoja na suala la muundo wa Muungano, maadili ya kijamii, uhuru wa kuabudu na uvumilivu wa dini nyingine.

## 13. Ardhi na Rasilimali

Ardhi ndiyo rasilimali asilia ya Watanzania wote na ndiyo msingi mkuu wa maisha yao. Inapendekezwa ardhi na mali asili za taifa viingizwe kwenye Mswada huu ili wananchi waweze kujadili ni mfumo gani wanataka wa kulinda na kumiliki ardhi na maliasili yao.

## 14. Maadili ya Kitaifa

Suala la maadili katika Mswada halijitoshelezi. Inapendekezwa suala la maadili ya kitaifa liainishwe kwenye Katiba kwani taifa lisilo na maadili ni taifa la waovu, vurugu na ufisadi. Sambamba na hilo kuna haja ya kuainisha maslahi ya Taifa ambayo kila mtanzania anawajibika kuyalinda.

## 15. Ushiriki wa Viongozi wa Dini kwenye mchakato

Inapendekezwa kwamba viongozi wa dini wapewe nafasi ya kushiriki katika mchakato wa Katiba kupitia umoja wao wa Baraza la Mashirikiano ya Dini Mbalimbali kwa ajili ya Amani Tanzania (Inter Religious Council for Peace Tanzania - IRCPT).